



Jaqueline Msuya  
Mhariri

## Karibuni Ulimwengu wa Elimu ya Juu 2026/2027

• Hatua Mpya, Fursa Mpya!



Mwaka wa masomo 2026/2027 unakaribia kufunguliwa rasmi mwezi Oktoba mwaka huu, ukiashiria safari mpya kabisa kwa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya kati na vya elimu ya juu nchini kote wakitokea kidato cha sita au ngazi ya stashahada.

Hali hii ya "upya" inajumuisha wanafunzi wanaokanyaga ardhi ya chuo kwa mara ya kwanza pamoja na wanafunzi waliokuwa chuoni lakini wamepata mkopo kwa mara ya kwanza. Kwa kuwa ugeni wa mazingira huambatana na kutokuwa na uzoefu wa taratibu mpya, HESLB inawahimiza wanafunzi wote waliopangiwa mikopo kuwa na kiu ya kujifunza taratibu za vyuo walivyodahiliwa na zaidi ya yote kuitambua na kuitembelea Ofisi ya Afisa Mikopo (Loan Officer) iliyopo katika kila chuo.

Ofisi hiyo ya mikopo ndiyo kiungo kikuu kati ya HESLB, mwanafunzi na chuo husika, na ndio maana wakati wa wiki ya mafunzo elekezi (orientation week), HESLB hutumia fursa hiyo kuwafikia wanafunzi moja kwa moja ili kutoa elimu kuhusu wajibu wao na matumizi sahihi ya fedha za mikopo.

Licha ya kwamba mnyororo mzima wa maombi hadi malipo hufanyika kwa njia ya mfumo wa kidijitali, ni muhimu sana kwa kila mwanafunzi mnufaika kufika katika ofisi ya mikopo chuoni mara tu anapowasili. Hatua hii inasaidia kuhakiki taarifa za msingi kabla ya kupokea mkopo, ikiwemo namba ya simu na akaunti ya benki, pamoja na kupata msaada au kufanya marekebisho yoyote yanayohitajika ili kuepuka ucheleweshaji wa malipo.

HESLB inamkumbusha kila mwanafunzi mnufaika wa mkopo wa elimu kuwa "Wewe Ndo Future" hivyo wote watimize wajibu wao na zaidi inawatakiwa kila la heri katika masomo yao wanufaika wote wapya wa mwaka wa masomo 2026/2027 na kuwakaribisha katika ngazi ya elimu ya juu.



## HESLB, CAMFED zasaini makubaliano kupanua fursa elimu ya Juu

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Shirika la Campaign for Female Education Tanzania (CAMFED), zimesaini Hati ya Makubaliano (MoU) yenye lengo la kuimarisha ushirikiano katika kuongeza upatikanaji wa rasilimali za kugharimia elimu ya juu kwa wanafunzi wenye uhitaji, hususan wasichana wanaotoka katika mazingira yenye changamoto za kiuchumi na kijamii.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini iliyofanyika Julai 2, 2026 katika Ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, amesema makubaliano hayo ni sehemu ya jitihada za Serikali za kutafuta mbinu bunifu za kuongeza vyanzo vya fedha vitakavyowezesha wanafunzi wengi zaidi kupata fursa za elimu ya juu.

"Serikali kupitia HESLB imeendelea kutafuta mbinu bunifu za kuongeza vyanzo vya fedha vitakavyosaidia wanafunzi wengi zaidi wenye sifa na uhitaji kupata fursa ya kuendelea na elimu ya juu. Makubaliano tunayoyasaini leo ni sehemu ya jitihada hizo," alisema Dkt. Kiwia.

Kwa mujibu wa Dkt. Kiwia, ushirikiano huo unalenga kuongeza upatikanaji wa fedha za kugharimia elimu ya juu, kupanua fursa kwa makundi yenye uhitaji mkubwa, kuongeza uelewa kuhusu huduma za HESLB, kuimarisha matumizi ya mfumo wa kidijitali, kubadilishana uzoefu wa kitaasisi na kujenga msingi wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi.

"Ushirikiano huu unaendana kikamilifu na dira yetu ya kuhakikisha hakuna mwanafunzi mwenye sifa anayekosa fursa ya elimu ya juu kwa sababu ya changamoto za kifedha," alisisitiza Dkt. Kiwia na kuongeza kuwa, "Tunatarajia ushirikiano huu utafungua ukurasa mpya wa uwezesaji wa elimu ya juu nchini. Kwa pamoja tunaweza kupanua fursa za elimu, kuwawezesha vijana wengi zaidi na kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa letu," alisema Dkt. Kiwia.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa CAMFED Tanzania, Bi. Anna Sawaki, alibainisha kuwa makubaliano hayo yanalenga kuwafikia watoto wengi zaidi wenye uhitaji wanaotoka katika mazingira magumu ili waweze kupata nafasi ya kuendelea na elimu ya juu.

"Tumekuwa tukifanya kazi na Bodi ya Mikopo kwa miaka mingi, na hivyo huu ni mwendelezo wa kazi ambayo tayari tulishaanza kwa miaka kadhaa... tunaahidi kuwa watekelezaji wazuri wa makubaliano haya na kutafuta vyanzo vingine vya kuongeza ufadhili kwa wanafunzi wahitaji kadri hali itakavyoruhusu," amesema Sawaki.

Makubaliano kati ya HESLB na CAMFED yanatarajiwa kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili katika kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za ziada, kuboresha uratibu wa programu za uwezesaji wa wanafunzi na kuongeza fursa za elimu ya juu kwa vijana wengi zaidi nchini, hususan wanaotoka katika mazingira yenye changamoto za kiuchumi na kijamii.

NDANI...



05

...NGORONGORO  
SCHOLARSHIP



08

SAIDI:  
KUTOKA MTWARA  
HADI DAR



**Mwenyekiti**  
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**  
Amani Kakana

**Mhariri**  
Jaqueline Msuya

**Wajumbe**  
Veneranda F. Malima  
Eline Maronga  
Ramadhan Namaru

**Designer**  
Saiki Visual Arts  
+255 621 579 833

**Photographer**  
Edwin Msuya  
+255 688 410 683

**Mawasiliano**  
Jengo la PSSSF,  
Barabara ya Makole,  
eneo la Uhindini  
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**  
+255 758 067 577  
+255 739 067 577

**Barua pepe:**  
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**  
www.heslb.go.tz

**HESLB**  
BODI YA MIKOPO  
INVESTING IN THE FUTURE

## MEZA YA MWENYEKITI



## KUFUNGWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA MIKOPO 2026/2027 NI MWANZO WA UPANGAJI MIKOPO

Dirisha la maombi ya mikopo kwa mwaka wa masomo 2026/2027 lilifunguliwa Juni 19, 2026 na kufungwa rasmi Septemba 18, 2026 ambapo vijana takriban 175,000 walipata fursa ya kujaza na kuwasilisha maombi yao kulingana na maelekezo kuhusu sifa na vigezo yaliyokuwa yametolewa kwenye mwongozo wa utoaji mikopo kwa mwaka husika. Maombi yalitaribishwa kutoka kategoria nne; shahada za awali, stashahada, stashahada ya juu ya uanasheria kwa vitendo na wanafunzi waliochaguliwa kupata ufadhili wa 'Samia Scholarship'.

Kufungwa kwa dirisha la maombi ya mikopo kwa mwaka wa masomo 2026/2027 ni mwanzo wa hatua nyingine muhimu katika kuhakikisha dhamira ya Serikali ya kutoa fursa sawa ya elimu ya juu inatimia kwa vijana wa kitanzania wenye sifa za kujiunga na elimu katika ngazi ya vyuo vya kati au taasisi za elimu ya juu.

Kwa niaba ya Menejimenti na watumishi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), napenda kuwapongeza kwa dhati wanafunzi wote waliokamilisha maombi yao ndani ya muda uliopangwa. Pia tunatoa shukrani kwa wazazi na walezi, taasisi za elimu ya juu, viongozi na wadau wote walioshiriki kuwahimiza na kuwawezesha waombaji kupata taarifa sahihi ili kukamilisha mchakato huu kwa usahihi na ukamilifu.

Sasa tunapoelekea hatua inayofuata, ni muhimu kwa waombaji kuelewa kuwa kufungwa kwa dirisha la maombi si mwisho wa safari; bali ni mwanzo wa mchakato wa uchambuzi na uhakiki wa taarifa na nyaraka walizowasilisha na kisha upangaji wa mikopo. Kama ilivyo

ada yetu, HESLB itaendelea kuchakata maombi kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa, kwa haki, uwazi na usawa, ili kuhakikisha rasilimali za Serikali zinawanufaisha wanafunzi wenye sifa na uhitaji.

Wakati mchakato ukiendelea, tunawashauri waombaji kuwa na subira na kuzingatia taarifa zinazotolewa kupitia njia rasmi za mawasiliano za HESLB ikiwemo tovuti [www.heslb.go.tz](http://www.heslb.go.tz). Mara awamu ya kwanza ya matokeo ya upangaji mikopo yatakapotangazwa, waombaji watapata taarifa kupitia akaunti zao walizoombea mikopo (SIPA) na kila mara watapewa maelekezo kuhusu hatua za kuchukua, ikiwemo taratibu za kukata rufaa kwa wale ambao watakuwa na sababu za kuomba mapitio ya upangaji au maamuzi ya awali.

Kwa upande wetu, Bodi itaendelea kusimamia mchakato huu kwa weledi na uwajibikaji, huku ikiboresha mifumo ya kidijitali kuwezesha huduma za mikopo ya wanafunzi kuwa rahisi zaidi, salama, za haraka na zinazomfikia kila mwanafunzi anayestahili.

Ni muhimu kwa wanafunzi kukumbuka kuwa Elimu ni msingi wa maendeleo ya mtu binafsi, familia na taifa kwa ujumla. Serikali kupitia HESLB itaendelea kuwa sehemu ya safari hiyo kwa kuhakikisha kwamba changamoto ya kutokuwa na uwezo wa kifedha haiwi kikwazo kwa kijana yeyote wa Tanzania mwenye sifa na anayestahili kupata elimu ya juu au katika chuo cha kati. Tunaamini katika kizazi chenye elimu, maarifa na ujuzi kitakacholiongoza Taifa letu kuelekea maendeleo endelevu, hivyo, kila hatua tunayochukua leo ni uwekezaji kuelekea Tanzania ijayo.

KUTOKA WIZARANI

ELIMU

UBUNIFU

UJUZI NA

“

Ushiriki wa HESLB ulilenga kuwafikia wanafunzi, wazazi, walezi na wananchi kwa ujumla ili kuwapatia taarifa sahihi kuhusu fursa za mikopo ya elimu ya juu, taratibu za maombi pamoja na wajibu wa wanufaika katika kurejesha mikopo yao kwa wakati.

”

## PROF. MKENDA AFUNGUA WIKI YA KITAIFA YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda amefungua rasmi Maonesho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu Agosti 18, 2026 katika viwanja vya Shule ya Sekondari Usagara, Jijini Tanga, yakilenga kuhamasisha na kuonesha mchango wa elimu, ujuzi na ubunifu katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Mhe. Prof. Mkenda alimwakilisha Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla ambapo pia viongozi mbalimbali wamehudhuria hafla hiyo ya ufunguzi akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian ambaye amewakaribisha wageni kutembelea vivutio mbalimbali vilivyomo mkoani humo ukiutaja Tanga kuwa ni 'lango la biashara la nchi za Afrika Mashariki na SADC'.

Katika maonesho hayo, yaliyoanza Agosti 15, 2026 na yalifika tamati Agosti 24, 2026, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilishiriki na kutoa elimu na uelewa kwa

wananchi na wadau mbalimbali kuhusu huduma inazotoa, hususan namna sahihi ya kuomba mikopo ya elimu ya juu pamoja na urejeshaji wa mikopo iliyoiva.

Ushiriki wa HESLB ulilenga kuwafikia wanafunzi, wazazi, walezi na wananchi kwa ujumla ili kuwapatia taarifa sahihi kuhusu fursa za mikopo ya elimu ya juu, taratibu za maombi pamoja na wajibu wa wanufaika katika kurejesha mikopo yao kwa wakati.

Maonesho hayo yaliyokuwa na kauli mbiu isemayo: "Elimu, Ujuzi na Ubunifu, Njia ya Kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050", yalitoa fursa kwa taasisi mbalimbali za elimu, wadau wa sekta ya elimu, wanafunzi na wananchi kukutana, kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu maendeleo ya elimu, ujuzi na ubunifu nchini.



## KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR ZAJIFUNZA HESLB

Wajumbe wa Kamati za Ustawi wa Jamii na Kamati ya Usimamizi wa Fedha (PSC) za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wamefanya ziara katika ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kujifunza na kupata uzoefu wa utekelezaji wa majukumu katika eneo hilo la Sekta ya elimu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, amesema ziara hiyo imewapa fursa ya kujifunza namna HESLB inavyosimamia fedha za elimu, matumizi ya teknolojia na mfumo wa urejeshaji wa Mikopo, na ameipongeza HESLB kwa kazi nzuri inayoifanya.

Katika ziara hiyo, wajumbe wa kamati hizo mbili walipata fursa ya kufahamu namna HESLB inavyosimamia utoaji wa mikopo na ufadhili wa wanafunzi, urejeshaji wa mikopo na matumizi ya mifumo ya kidigitali katika kuboresha huduma.

Awali, akitoa wasilisho kuhusu muundo na utekelezaji wa majukumu ya HESLB, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi hiyo, Dkt. Bill Kiwia, alisema HESLB ilianzishwa mwaka 2004 kwa Sheria na inatekeleza majukumu makuu mawili ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji pamoja na kukusanya fedha kutoka kwa wanufaika ambao madeni yao yameiva.

Dkt. Kiwia alisema kwa mwaka wa masomo 2026/2027, serikali imetenga TZS 1.07 trilion kwa ajili ya mikopo na ufadhili, unaolenga kuwanufaisha wanafunzi 292,463, wakiwemo wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo.

Wengine walioandamana na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizo mbili za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni pamoja na viongozi wa taasisi na maafisa wa Wizara ya Elimu ya Muungano (WyEST) na Wizara ya Elimu Zanzibar (WEMA) wakiongozwa na Naibu Waziri wa WEMA, Mhe. Khadija Salum Ali ambaye amesema ziara hiyo imekuwa ya manufaa makubwa.

“Waheshimiwa Wenyevidi na Wawakilishi, nadhani mmeona faida ya ziara hii ... tulivyokuja sivyo tutakavyoondoka”, amesema Mhe. Khadija.

Ziara hiyo ni sehemu ya jitihada za kujifunza na kubadilishana uzoefu katika usimamizi wa sekta ya elimu, ambapo Wajumbe walieleza kuwa maarifa waliyoyapata HESLB yatakuwa sehemu ya uzoefu watakaotumia katika kuimarisha usimamizi wa elimu na rasilimali zake Zanzibar.

“

kuhusu muundo na utekelezaji wa majukumu ya HESLB, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi hiyo, Dkt. Bill Kiwia, alisema HESLB ilianzishwa mwaka 2004 kwa Sheria na inatekeleza majukumu makuu mawili ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji pamoja na kukusanya fedha kutoka kwa wanufaika ambao madeni yao yameiva.

”

# WANAFUNZI 15 KUNUFAIKA NA 'NGORONGORO SCHOLARSHIP'

Wanafunzi 15 wanaotoka katika jamii zinazoishi ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro wanatarajiwa kunufaika na ufadhili maalum wa elimu ya juu huku Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ikitenga TZS 99 milioni kugharimia masomo yao kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

Hayo yalibainishwa Agosti 4, 2026, jijini Dar es salaam wakati Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) zilipozindua rasmi Mwongozo wa Utoaji wa 'Ngorongoro Scholarship', hatua iliyoashiria kuanza kwa ufadhili maalum wa elimu ya juu kwa wanafunzi wanaotoka katika jamii zinazoishi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kuanzia mwaka wa masomo 2026/2027.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia, alisema uzinduzi huo ni utekelezaji wa Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) yaliyosainiwa kati ya HESLB na NCAA tarehe 24 Oktoba, 2025, lengo kuu likiwa ni kuongeza fursa za elimu ya juu kwa vijana wa eneo la Ngorongoro.

"Kuanzia mwaka wa masomo 2026/2027, HESLB kwa kushirikiana na NCAA itaanza kutoa ufadhili maalum wa elimu ya juu. Hatua hii ni uwekezaji muhimu katika rasilimali watu na maendeleo endelevu ya Taifa kupitia elimu," alisema Dkt. Kiwia.

Aliongeza kuwa mwongozo huo umeweka vigezo na taratibu za utoaji wa ufadhili ambao utaanza kwa wanafunzi wa fani zinazohusiana na uhifadhi wa wanyamapori, misitu, malikale na utalii, huku wigo ukitarajiwa kupanuliwa kadiri mfuko utakavyoendelea kukua, huku dirisha la maombi likifunguliwa rasmi tarehe 15 Agosti, 2026 kuruhusu waombaji wenye sifa kuwasilisha maombi yao kupitia mfumo wa kidijitali ulioboreshwa na HESLB.


Kwa upande wake, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi wa NCAA, Bi. Gloria Bideberi, alisema mpango huo unaonesha dhamira ya NCAA ya kuwekeza katika maendeleo ya jamii kupitia elimu sambamba na kuimarisha juhudi za uhifadhi.

"Ngorongoro Scholarship inaashiria dhamira ya NCAA ya kuwekeza katika rasilimali watu kupitia elimu. Tunaamini maendeleo ya uhifadhi hayawezi kutenganishwa na maendeleo ya watu, ndiyo maana tumeamua kushirikiana na HESLB kuhakikisha kila mwanafunzi anayekidhi vigezo anapata fursa ya kufadhiliwa," alisema Bi. Bideberi.

Alibainisha kuwa NCAA imekuwa ikiwezesha elimu kwa watoto wa jamii za Ngorongoro kwa zaidi ya miongo mitatu, ambapo hadi mwaka wa fedha 2025/2026 zaidi ya wananchi 15,000 walikuwa wamepatiwa ufadhili katika taaluma mbalimbali. Aidha, alisema kupitia 'Ngorongoro Fund' yenye kauli mbiu isemayo "Elimu Endelevu kwa Maendeleo ya Jamii na Uhifadhi".

HESLB na NCAA zimetoa wito kwa wazazi, walezi, viongozi wa jamii na vijana kutumia fursa hiyo kwa kuwasilisha maombi mara tu dirisha litakapofunguliwa, huku pia zikizihamasisha taasisi mbalimbali na wadau wa maendeleo kuunga mkono mfuko huo ili kuongeza idadi ya wanufaika katika miaka ijayo.





# BoT NA HESLB WAZINDUA UFADHILI WA MASOMO KUMWADHIMISHA NYERERE

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mhe. Emmanuel Tutuba, akishirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia, wamezindua rasmi Mwongozo wa Ufadhili wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mpango wenye lengo la kuwawezesha wanafunzi mahiri wa Kitanzania kupata shahada za uzamili katika fani muhimu za maendeleo ya Taifa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo uliofanyika Agosti 28, 2026, jijini Dar es Salaam, Gavana Tutuba alisema kuwa mpango huo unawazingatia wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili, katika fani za Sayansi, Hisabati, Uchumi, TEHAMA, na Uhasibu. Alieleza kuwa katika mwaka wa masomo 2025/2026, BoT ilitoa ufadhili kwa wanafunzi 100, na kwa mwaka wa masomo 2026/2027 inatarajiwa kutoa ufadhili kwa wanafunzi 10, wakiwemo watatu wa Shahada ya Uzamili na saba wa Shahada ya Awali.


Kwa upande wake, Dkt. Kiwia alisema, kukabidhiwa jukumu la kutangaza na kupokea maombi ya ufadhili huo ni ishara ya imani kubwa ambayo BoT imeijenga kwa HESLB kutokana na uwezo wake wa kusimamia ufadhili kwa ufanisi, uwazi na uwajibikaji. Dkt. Kiwia alisisitiza

umuhimu wa matumizi ya teknolojia katika kurahisisha upatikanaji wa fursa za elimu, akieleza kuwa HESLB imeendelea kuwekeza katika mifumo ya kidijitali inayomwezesha mwanafunzi kuomba ufadhili kwa muda mfupi na kwa urahisi zaidi.

Wanafunzi watakoachaguliwa watapatiwa ufadhili wa asilimia 100 unaogharimia ada ya masomo pamoja na mahitaji mengine ya mwanafunzi kwa kuzingatia muundo wa gharama wa taasisi husika. Maombi yote yamefanyika kupitia Mfumo wa Maombi ya Mikopo wa HESLB (OLAMS) kuanzia Septemba 5 hadi Oktoba 5, 2026.

Ufadhili huo ulianzishwa na BoT mwaka 2009 kwa lengo la kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na kuendeleza dhamira yake ya kutumia elimu kama nyenzo muhimu ya kujenga rasilimaliwatu na kuchochea maendeleo ya Taifa.

Mpango huu ufadhili wa masomo unaendelea kuakisi umuhimu wa kuwekeza kwa vijana wenye uwezo wa kitaaluma katika fani zinazohitajika, huku ushirikiano kati ya BoT na HESLB ukihakikisha fursa hizi zinawafikia wanaostahili kwa njia ya uwazi na ufanisi.



## NAIBU KAMISHNA MIKOPO NA UFADHILI TAHLISO ATEMBELEA HESLB

Naibu Kamishna wa Mikopo na Ufadhili kutoka Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu (TAHLISO), Bi. Agnes Kado, ametembelea Ofisi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) zilizopo Dodoma, kwa lengo la kujitambulisha rasmi na kukutana na maafisa wa Bodi.

Ziara hiyo iliyofanyika Julai 14, 2026, ni sehemu ya kuimarisha ushirikiano kati ya TAHLISO na HESLB katika kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya juu wanaendelea kupata fursa na huduma bora za mikopo na ufadhili.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Bi. Kado ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. John's kilichopo Dodoma, amesema anatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na HESLB katika kuwawezesha wanafunzi wengi wenye sifa kutimiza ndoto zao za elimu ya juu kupitia huduma za mikopo na ufadhili.

Aidha, kwa niaba ya uongozi wa TAHLISO, ametoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Mikopo kwa kazi nzuri na yenye tija inayofanya katika kuwahudumia wanafunzi na kuchangia maendeleo ya taifa.

Ziara hiyo imeonesha dhamira ya dhati ya pande zote mbili katika kuendeleza ushirikiano wenye manufaa na tija kwa wanafunzi wa elimu ya juu na wadau wa sekta ya elimu nchini.

“

Anatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na HESLB katika kuwawezesha wanafunzi wengi wenye sifa kutimiza ndoto zao za elimu ya juu kupitia huduma za mikopo na ufadhili

”



## SAIDI: Kutoka Mtwara hadi Dar

Ndoto ya kijana Saidi Muksini Adamu kupata elimu ya juu imeanza kutimia baada ya kunufaika na mkopo wa elimu ya juu unaotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Saidi mwenye ulemavu kutoka Kata ya Ziواني, Wilaya ya Mtwara Vijijini, ni mwanafunzi wa mwaka wa pili wa Shahada ya Awali ya Usimamizi wa Raslimaliwatu katika Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA), Kampasi ya Dar es Salaam. Akiwa ametoka katika familia yenye uwezo mdogo wa kiuchumi, amesema mkopo wa HESLB umekuwa msaada mkubwa katika kumwezesha kuendelea na masomo na kufikia ndoto yake.

"Ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia HESLB kwa kunipatia mkopo. Bila mkopo huu, kwa hali ya familia yangu, ingekuwa vigumu sana kufika hapa nilipo," alisema Saidi katika mahojiano maalumu na HESLB Yako.

Mama yake, Bi. Khadija Mfaume, ameishukuru Serikali kwa kumwezesha mwanawe

kupata elimu ya juu, akisema familia yao isingekuwa na uwezo wa kugharimia masomo yake bila msaada huo.

Kutokana na kunufaika na mkopo huo, Saidi ametoa wito kwa wanufaika ambao mikopo yao imeiva na wana uwezo wa kurejesha, kufanya hivyo ili kuwawezesha vijana wengine wenye sifa na uhitaji kupata fursa kama aliyopata yeye.

"Nawasihi wanufaika wenzangu ambao mikopo yao imeiva na wana kipato waanze kurejesha. Hata kama kipato ni kidogo, unaweza kuanza na Shilingi 5,000 na kuendelea. Kidogo kidogo deni linaisha. Tunaporejesha mikopo yetu, tunaiwezesha HESLB kuwafikia vijana wengine wenye uhitaji. KIDUCHU, Fresh tu – Tunasonga tu!" amesema Saidi.

Kampeni ya HESLB ya "KIDUCHU – Fresh tu, Tunasonga tu", iliyozinduliwa Aprili mwaka huu, inamlenga mnufaika mwenye kipato kidogo ili aweze kuanza kurejesha deni lake kidogo kidogo, kuanzia TZS 5,000 na kuendelea, ili hatimaye amalize kulipa deni lake.

# MULIRO: HONGERENI HESLB KWA UBUNIFU WA “KIDUCHU” NA MAGEUZI YA KIDIJITALI

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Jumanne Muliro, ameipongeza HESLB kwa kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, kuimarisha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo na kubuni kampeni ya urejeshaji kidogokidogo maarufu Kiduchu, ambao amesema utasaidia kuongeza ushiriki wa wadaiwa kurejesha mikopo ya elimu ya juu.

SACP M.J Muliro ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la HESLB katika siku ya kilele cha Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Akiwa katika banda hilo, SACP M.J Muliro amesema HESLB imeendelea kuonesha dhamira ya kuhakikisha fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu zinawanufaisha Watanzania wengi zaidi kwa kusimamia ipasavyo urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wenye kipato waliohitimu masomo yao na kuajiriwa au kujiajiri.

Amesema juhudi za kuwafuatilia wadaiwa na kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kurejesha mikopo ni hatua muhimu inayoweza fedha hizo kuendelea kuwanufaisha wanafunzi wengine wanaostahili kupata mikopo kwa ajili ya kuendelea na masomo ngazi ya elimu ya juu.

Aidha, Kamanda Muliro ameipongeza HESLB kwa kuanzisha kampeni ya Kiduchu, akieleza kuwa ni ubunifu unaotoa nafasi kwa wadaiwa wenye vipato vya chini kuanza kurejesha mikopo yao kulingana na uwezo wao, hatua itakayoongeza hamasa ya urejeshaji na kuimarisha uendeleu wa mfuko wa mikopo ya elimu ya juu.

“Huu ni ubunifu mzuri ambao unawapa fursa hata wale wenye kipato kidogo kuanza kutekeleza wajibu wao wa kurejesha mikopo. Hii itaongeza mwtikio wa wadaiwa na kuwafanya wengi zaidi washiriki katika kuchangia elimu ya vizazi vijavyo,” alisema SACP M.J Muliro.

Kamanda Muliro ameisifu HESLB kwa kuendelea kuboresha huduma zake mwaka hadi mwaka kupitia matumizi ya teknolojia ya kidijitali, akibainisha kuwa hatua hizo zimeongeza ufanisi, uwazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muliro amewataka wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutambua kuwa kurejesha mikopo ni wajibu wa kila mnufaika, akisisitiza kuwa urejeshaji huo unawezesha wanafunzi wengine kupata fursa ya elimu ya juu,



## MHE. FERUZI

### AIPONGEZA HESLB KUTHIBITISHWA KIWANGO CHA KIMATAIFA

Mbunge wa Viti Maalumu anayewakilisha Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu, Mhe. Asha Feruzi, ameipongeza HESLB kwa kufanikiwa kuthibitishwa kwa kiwango cha kimataifa cha usimamizi wa ubora, ISO 9001:2015, akieleza kuwa mafanikio hayo ni kielelezo cha dhamira ya taasisi hiyo katika kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Feruzi ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la HESLB katika maonesho ya 50 ya Sabasaba na kujionea namna elimu kuhusu utoaji na urejeshaji wa mikopo inavyotolewa, akisema pamoja na kupata uthibitisho huo wa kimataifa, ni muhimu kwa watumishi wa HESLB kuendelea kuzingatia weledi, uwajibikaji na utoaji wa huduma zenye viwango vya juu ili kuendelea kujenga imani ya wananchi na kuongeza ufanisi wa taasisi hiyo.

Mhe. Feruzi ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, pia aliipongeza HESLB kwa kuendelea kufanya maboresho ya huduma zake kupitia matumizi ya teknolojia za kisasa, hatua ambayo alisema imerahisisha upatikanaji wa taarifa na kusogeza huduma karibu zaidi kwa wadau wa elimu.

Alieleza kuwa maboresho hayo yatasaidia kupunguza changamoto na makosa ambayo yamekuwa yakijitokeza

mara kwa mara wakati wa maombi ya mikopo kila mwaka na kuongeza kuwa utoaji elimu kupitia njia mbalimbali, ikiwemo mitandao ya kijamii na majukwaa ya kuwafikia walengwa moja kwa moja, unaonesha dhamira ya dhati ya HESLB ya kuhakikisha hakuna mwanafunzi mwenye sifa ya kupata mkopo anayekosa fursa kutokana na kukosa baadhi ya taarifa.

"Hii ni ishara kwamba HESLB imejipanga kuhakikisha kila mwanafunzi mwenye uhitaji anapata fursa ya kutimiza ndoto zake kielimu kupitia taarifa sahihi na huduma zinazomfikia kwa wakati," alisema.

Mhe. Feruzi alihitimisha kwa kusema kuwa juhudi za HESLB katika kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa njia za kidijitali zina mchango mkubwa katika kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi wanafikiwa kwa wakati na kwa ufanisi.

Ziara ya Mhe. Feruzi ilionesha umuhimu wa ushirikiano kati ya viongozi na taasisi za elimu katika kuendelea kuboresha huduma kwa wanafunzi, ili kuhakikisha kila mwenye sifa na uhitaji anapata fursa ya kufikia malengo yake ya elimu na kuchangia maendeleo ya Taifa.

“

"Hii ni ishara kwamba HESLB imejipanga kuhakikisha kila mwanafunzi mwenye uhitaji anapata fursa ya kutimiza ndoto zake kielimu kupitia taarifa sahihi na huduma zinazomfikia kwa wakati,"

”

## KAMERA YETU



**Julai 13, 2026, Dar es Salaam:** Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwira (katikati), pamoja na watumishi kutoka HESLB baada ya kupokea tuzo ya mshindi wa kwanza wa Banda Bora la Sekta ya Elimu, kwenye hafla ya kufunga Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF).



**Agosti 04, 2026, Dar es Salaam:** Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia (wa tatu kushoto), Mkurugenzi wa Utoaji Mikopo (HESLB) Dkt. Peter Mmari (wa kwanza kulia) pamoja na Madafisa kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwenye uzinduzi wa Mwongozo wa Ngorongoro 'Scholarship'.




**Agosti 28, 2026, Dar es Salaam:** Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba (kulia), na Mkurugenzi Mfundaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia, wakizindua mwongozo wa Ufadhili wa Shahada ya Uzamili ya Kumbukumbu Mwalimu Julius K. Nyerere.



**Agosti 31, 2026, Dar es Salaam:** Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar (WEMA), Mhe. Khadija Salum Ali (katikati mstari wa kwanza), pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenye picha ya pamoja walipotembelea ofisi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), kulia kwa Naibu Waziri ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwira.



**Septemba 02, 2026, Mwanza:** Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Prof. Hamisi Dihenga (aliyekaa katikati), akiwa na baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi waliomaliza muda wao katika hafla tupi iliyoambatana na vikao maalum kati ya Menejimenti ya HESLB na Bodi ya Wakurugenzi.



**Septemba 07, 2026, Morogoro:** Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi (katikati), kwenye picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bili Kiwira.

## KIONGOZI WA VISA A/MASHARIKI NA KATI ATEMBELEA HESLB

Kiongozi Mkuu wa Mashirikiano na Wadau wa Kampuni ya VISA Kanda ya Kati na Mashariki mwa Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika (CEMEA), Bw. Athman Ali, ametembelea Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya HESLB, jijini Dar es salaam na kukutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia.

Ujio wa kiongozi huyo wa VISA ulilenga kujadili fursa za ushirikiano kati ya HESLB na VISA katika kuboresha mifumo ya utoaji na usimamizi wa fedha za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kutumia teknolojia za kisasa za huduma za kifedha.

Katika mazungumzo hayo, pande zote mbili zilijadili namna ya kutatua changamoto zinazohusiana na matumizi ya fedha za mikopo, hususan kuhakikisha fedha

zinazotolewa kwa wanufaika zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, ikiwa ni pamoja na kugharimia mahitaji muhimu ya masomo na ustawi wa mwanafunzi akiwa chuoni.

Aidha, viongozi hao walisisitiza umuhimu wa kutumia suluhisho za kidijitali zitakazoongeza uwazi, usalama na ufanisi katika usimamizi wa fedha za mikopo, sambamba na kuwajengea wanafunzi utamaduni wa matumizi sahihi ya huduma za kifedha.

Ushirikiano kati ya HESLB na VISA unatarajiwa kuibua fursa mpya za kuboresha utoaji wa huduma kwa wanufaika wa mikopo, kuhakikisha fedha za umma zinatumiwa kwa tija na kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuimarisha upatikanaji wa elimu ya juu nchini.

“

Ujio wa kiongozi huyo wa VISA ulilenga kujadili fursa za ushirikiano kati ya HESLB na VISA katika kuboresha mifumo ya utoaji na usimamizi wa fedha za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kutumia teknolojia za kisasa za huduma za kifedha

”



“Hongereni sana kwa makusanyo makubwa katika mikopo iliyoiva. Kwa kweli mnastahili pongezi kubwa sana

## KM - WyEST AIPONGEZA HESLB KWA UTOAJI ELIMU NA MIKOPO ILIYOIVA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), Prof. Carolyne Nombo, Prof. Nombo ameipongeza Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa juhudi inazozifanya katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna sahihi ya kuomba mikopo ya elimu ya juu, pamoja na kuelimisha wanufaika kuhusu umuhimu wa kurejesha kwa wakati mikopo iliyoiva

Prof. Nombo aliyasema hayo alipotembelea banda la HESLB katika maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu 2026 yaliyofanyika Agosti 15, 2026 hadi Agosti 24, 2026 katika viwanja vya Shule ya Sekondari Usagara, jijini Tanga.

Aidha, Prof. Nombo ameipongeza HESLB kwa mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa marejesho ya mikopo ya wanafunzi, akieleza kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kuhakikisha Mfuko wa Mikopo unakuwa endelevu na kuwafikia wanafunzi wengi zaidi wenye sifa na uhitaji.

“Hongereni sana kwa makusanyo makubwa katika mikopo iliyoiva. Kwa kweli mnastahili pongezi kubwa sana,” alisema Prof. Nombo.

Katibu Mkuu wa WyEST pia alisisitiza umuhimu wa HESLB kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia maonesho na majukwaa mbalimbali ili kuongeza uelewa kuhusu fursa za mikopo, taratibu za maombi na wajibu wa wanufaika kurejesha mikopo yao kwa wakati.

Maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu 2026 yalitumika kama jukwaa la pamoja kwa taasisi na wadau wa elimu kuonesha huduma, ujuzi na ubunifu ili kutangaza fursa zinazopatikana katika sekta ya elimu.



# Dkt. Kiwia:

## Shukrani zangu kwenu Bodi ya Wakurugenzi HESLB Iliyomaliza Muda

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Dkt. Bill Kiwia, ametoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB iliyomaliza muda wake, akieleza kuwa ushirikiano mzuri na uongozi wa Bodi hiyo umeiwezesha HESLB kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kufikia malengo yake ya kimkakati katika kipindi cha miaka mitatu (2023 - 2026).

Dkt. Kiwia ametoa shukrani hizo wakati wa hafla fupi iliyoambatana na vikao maalum kati ya Menejimenti ya HESLB na Bodi ya Wakurugenzi vilivyofanyika tarehe 01 na 02 Septemba, 2026 katika Hoteli ya Malaika, jijini Mwanza.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dkt. Kiwia alisema Bodi hiyo imekuwa ya kipekee kutokana na ushirikiano wake wa karibu na Menejimenti, jambo lililowezesha Menejimenti ya HESLB kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuongeza ufanisi ikiwemo utoaji wa mikopo na kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi wenye uhitaji wananufaika na fursa za kupata elimu ya juu.

"Kwa niaba ya Menejimenti na watumishi wote wa HESLB, ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi kwa ushirikiano wenu wa karibu, ushauri na uongozi mliutoa katika kipindi chote cha uongozi wenu. Bodi hii imekuwa ya kipekee na imeiwezesha HESLB kutekeleza mikakati muhimu ya kuongeza idadi ya

wanafunzi wanaonufaika na mikopo, huku tukijenga msingi wa kuwa na mfuko endelevu wa mikopo," alisema Dkt. Kiwia.

Aliongeza kuwa, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wa Bodi hiyo yenye wajumbe 9 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wanaowakilisha maeneo ya sheria, fedha, elimu ya juu na elimu ya kati, ni matokeo ya ushirikiano, uongozi thabiti na maamuzi ya kimkakati yaliyolenga kuimarisha huduma zinazotolewa na HESLB kwa wanafunzi na wadau wake.

Dkt. Kiwia aliwashukuru Wajumbe wa Bodi hiyo wakiongozwa na Mwenyekiti wake Prof. Hamisi Dihenga kwa kujitolea kwao, weledi na usimamizi madhubuti, akisema Menejimenti inathamini mchango wa kila mmoja katika kuhakikisha HESLB inatimiza dhamana yake ya kuwezesha wanafunzi wa Kitanzania kupata elimu ya juu kupitia mikopo na ruzuku.

Hafla hiyo ilikuwa ni sehemu ya kushukuru, kutambua, kuthamini na kuaga kwa heshima Bodi ya Wakurugenzi iliyomaliza muda wake, huku Menejimenti ya HESLB ikieleza utayari wa kuendeleza misingi mizuri ya utendaji na mikakati iliyowekwa kwa manufaa ya wanafunzi na ustawi wa HESLB.



## WANAFUNZI WA KISARAWA SEMINARI WAJENGEWA UELEWA WA KINA KUELEKEA ELIMU YA JUU

Wanafunzi wa Kidato cha Sita kutoka shule ya Kisarawe Seminari (Kisarawe Lutheran Junior Seminary) wametembelea ofisi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) jijini Dar es Salaam, ambapo wamepata fursa ya kujifunza na kupata uelewa wa kina kuhusu mchakato mzima wa uombaji wa mikopo ya elimu ya juu pamoja na urejeshaji wa mikopo iliyoiva.

Wanafunzi hao, kutoka tahasusi mbalimbali za masomo zikiwemo PCB, PCM, EGM na HGL walipokelewa na kupatiwa mafunzo ya hatua kwa hatua kuhusu namna HESLB inavyotekeleza majukumu yake katika kuwezesha wanafunzi wenye sifa kupata fursa ya kujiendeleza kimasomo.

Pamoja na mambo mengine, wanafunzi hao walielekezwa taratibu zote za maombi ya mikopo kuanzia dirisha la maombi linapofunguliwa, namna ya kuwasilisha maombi na taarifa muhimu, hatua za uchakataji na uhakiki, hadi kufikia hatua ya kupangiwa na kutolewa kwa fedha za mikopo kwa wanafunzi wanaokidhi vigezo.

Mbali na elimu ya uombaji mkopo, wanafunzi hao walipata pia elimu kuhusu urejeshaji wa mikopo iliyoiva na kuelewa kwa kina kuhusu wajibu wa mnufaika kuanza kurejesha mkopo pindi anapokamilisha masomo yake ya elimu ya juu.

Aidha, walifahamishwa kuhusu umuhimu wa kutambua kuwa fedha za mikopo ni uwezeshaji unaopaswa kurejeshwa ili kuwezesha wanafunzi wengine wwanaojiunga na elimu ya juu kunufaika.

Akizungumzia manufaa ya ziara hiyo, Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Kisarawe Seminari, Brian Charles Urio, alieleza kuwa ziara hiyo imewasaidia kuondokana na dhana au taarifa zisizo sahihi ambazo zimekuwa zikienea mtaani kuhusu vigezo na taratibu za mikopo ya elimu ya juu ikiwa ni pamoja na madai kwamba wanafunzi waliosoma shule binafsi kama wao, hawana nafasi ya kupangiwa mikopo.

"Tumefurahi sana kupata nafasi hii ya kutembelea HESLB. Tulichokiona katika utendaji kazi na elimu tuliopata hapa ni tofauti na baadhi ya taarifa tunazozisikia mtaani. Tumepewa elimu ya moja kwa moja na tumeelimishwa namna mchakato wa mikopo unavyofanyika ... maarifa haya yatatusaidia kufanya maamuzi sahihi tunapofikia hatua ya kuomba mikopo na pia kuwaelimisha wenzetu," alisema Urio.

Wanafunzi hao pia wameahidi kuwa mabalozi wazuri wa HESLB kwa kuwafikishia wenzao na jamii kwa ujumla taarifa sahihi kuhusu mikopo ya elimu ya juu, hususan katika kipindi ambacho taarifa potofu zinaweza kuwafanya baadhi ya wanafunzi kukata tamaa au kufanya maamuzi yasiyo sahihi.

Wametambua zaidi kwamba ziara ya HESLB haikuwa tu matembezi ya kielimu, bali ilikuwa darasa la vitendo lililowapa mwanga kuhusu safari yao ya elimu ya juu na namna wanavyoweza kunufaika na huduma za mikopo kwa uelewa sahihi na uwajibikaji.



## WANAFUNZI 34 WAIFIKISHA TANZANIA HATUA MPYA KWENYE TEKNOLOJIA

Wanafunzi 34 ambao wamebeba ndoto kubwa ya Taifa Kutoka madarasani Tanzania hadi kwenye uwanja wa kimataifa wa teknolojia kupitia Samia Scholarship Extended DS/AI+—ikiwa ni fursa inayolenga kuandaa kizazi kitakacholeta fursa na mtazamo chanya katika dunia ya teknolojia.

Wanafunzi hao 34 ni kati ya wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi, wamekwenda nchini Ireland kusoma programu za sayansi ya data na akili unde [Data Science, Artificial Intelligence (AI)] na fani shirikishi, huku wanafunzi 16 tayari wakiwa wameshaenda nchini Afrika Kusini na wanaendelea na masomo.

Kundi hilo linajumuisha wanafunzi 50 waliofanya vizuri katika masomo ya sayansi katika Kidato cha Sita mwaka 2024/2025, pamoja na 10 waliofanya vizuri mwaka 2025/2026, ambao wamepata fursa kupitia mpango huo wa ufadhili.

Wanafunzi hao waliwekwa kwenye kambi maalumu (boot camp) katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela iliyopo Arusha ambapo walipewa mafunzo na elimu ya jinsi ya kuishi ugenini. Sambamba na hilo, walisisitizwa kuwa na uzalendo, kujiamini na kupenda nchi yao.

Kwa Serikali ya Tanzania, hatua hii ni zaidi ya kuwapeleka vijana kusoma nje ya nchi, ni uwekezaji katika kizazi kijacho cha wataalamu wa teknolojia, wabunifu na wazalishaji wa maarifa, watakaotumia ujuzi wao kutengeneza suluhisho na kuchochea maendeleo ya Taifa ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Tanzania kuwa na wataalamu wenye uwezo wa kushindana na kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali na dunia ya maarifa.

“

Wanafunzi hao waliwekwa kwenye kambi maalumu (boot camp) katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela iliyopo Arusha ambapo walipewa mafunzo na elimu ya jinsi ya kuishi ugenini. Sambamba na hilo, walisisitizwa kuwa na uzalendo, kujiamini na kupenda nchi yao.

”

## WASILIANA NASI:

### DODOMA

Jengo la PSSSF,  
Br. Makole, eneo la  
Uhindini  
S.L.P 984, Dodoma  
Simu +255 758 067577  
+255 739 06757  
Barua Pepe:  
info@heslb.go.tz

### ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,  
Ghorofa ya Kwanza  
S.L.P 2712, Arusha  
Simu: 027 2520128  
0624 100 011  
0739 102 016  
Barua Pepe:  
arusha@heslb.go.tz

### MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa  
ya pili Br. Kenyatta  
S.L.P 3051, Mwanza  
Simu: 028 2506008  
0759 819 350  
0738 153 661  
Barua Pepe:  
mwanza@heslb.go.tz

### ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,  
Eneo la Michenzani  
Ghorofa ya Tano  
S.L.P 900, Zanzibar,  
Simu: 0779 321 424  
Barua Pepe:  
zanzibar@heslb.go.tz

### HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower  
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni  
S.L.P 76068, Dar es Salaam  
Simu: +255 758 067 577  
+255 739 067 577  
Barua Pepe:  
info@heslb.go.tz

### MBEYA

Jengo la CAG, Ghorofa ya  
Nne, Br. Mbalizi  
S.L.P 319, Mbeya  
Simu: 0738 131 310  
0738 131 311  
Barua Pepe:  
mbeya@heslb.go.tz

### MTWARA

NHC Raha Leo Complex,  
Ghorofa ya tatu,  
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu  
na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa  
S.L.P: 969, Mtwara.  
Simu: +255 733 068 171  
Barua Pepe:  
mtwara@heslb.go.tz

### DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya  
Wanafunzi wa Elimu ya Juu,  
1 Mtaa wa Kilimo, Tazara,  
Br. Mandela  
S.L.P 76068,  
15471-Dar Es Salaam  
Simu: 0736 665 533  
Barua Pepe:  
info@heslb.go.tz

